102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA FASIHI

TATHMINI YA PAMOJA MACHI/APRILI 2017

SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

(a)i Utungo wa kishairi ambao hutungolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na

uzungumzaji (kalima) 1 x 2 =alama 2

(ii) Sifa za maghani

(i) Yana muundo wa kishairi.

(ii) Tamathali za semi hutumika kwa wingi.

(iii) Huganiwa katika sherehe za kijamii.

(iv) Hutumia kiimbo cha juu yanaposemwa.

(v) Huwa na uigizaji au utendaji.

(vi) Hutawaliwa na majisifu na majigambo.

(vii) Husifia mambo /vitu vinavyoleta sifa katika jamii.

(viii) Hukashifu wapinzani wa mashujaa katika jamii.

(ix) Maghani hutungwa papo hapo na kutongolewa mbele ya hadhira.

(x) Huweza kutongolewa na mtu mmoja au kundi la watu.

Zozote nne 4 x 2 = alama 8

(b)i maana ya vitanza ndimi-kauli zenye maneno ambayo yana mfuatano wa sauti zinazotatanisha kimatamshi./mchezo wa maneno yanayokanganya kimatamshi kwa sababu ya kukaribiana kisauti.(al 2)

(ii) dhima/umuhimu

- Hukuza matamshi bora.
- Hukuza uwezo wa kufikiria haraka.
- Huhifadhi utamaduni na kuurithisha.

- Ni kitambulisho cha jamii husika.
- Hukuza ubunifu kwani anayevibuni sharti awe na ujuzi mpana wa lugha.
- Huburudisha kwa kuzua ucheshi.
- Ni njia moja ya kuwajengea vijana msingi bora wa kuwa wasemaji hodari wa baadaye.

Zozote 4 x 2 = 8

SEHEMU YA B: TAMTHILIA

2.a) Mneneji –Waridi

Mnenewa – Daktari Siki.

Mahali – ofisi ya Siki

Ni baada ya Waridi kukiri kuwa ahadi ya Meya kuwa dawa zilikuwa njiani ulikuwa uongo.

(hoja 4 x 1 = 4)

b)Sababu za Waridi za kuacha kazi

- Kufiwa na mtoto wa mamake mdogo mikononi mwake tutokana na ukosefu wa dawa.
- Kutolipwa nusu ya mshahara wa mwezi uliotangulia.
- Waridi anaona kazi hiyo haimfaidi yeye binafsi wala watu wengine.
- Uchafu ulio hospitalini unahatari maisha yao.
- Kuna fununu kuwa kutakuwa na maandamano au mgomo.

(hoja 5 x 2 = 10)

c)Mnenewa ni Siki

Sifa zake

- Jasiri
- Mwenye utu
- Mzalendo
- Mwenye matumaini
- Anayewajibika kazini
- Mkweli
- Aliyezinduka kisiasa.
- Mshauri mwema

(hoja 6 x 1 = 6)

Umuhimu wa Siki

- Kielezo cha wafanyikazi wa umma waadilifu.
- Anatumiwa na mwandishi kumwambia Meya ukweli ambao madiwani hawamwambii.
- Ni kielelezo cha utu/ wema katika jamii.
- Mwandishi anamtumia kukuza maudhui ya :utu, uazalendo, miongoni mwa mengine.
- Kupitia kwake sifa za baadhi ya wahusika zinabainika km Waridi, Meya, tatu na Diwani III.
- Anawakilisha wanataluuma ambao hususia siasa ati ni mchezo mchafu.

(hoja 4 x 1 = 4)

3.Tamthilia ya **Mstahiki Meya** inasawiri picha halisi ya mataifa mengi barani Afrika. Dhihirisha. (al.20)

Tamthilia ya Mstahiki meya inaafiki mataifa ya Kiafrika kwa sababu matukio mengi katika kitabu ni:

- ufisadi
- umasikini
- ukoloni mamboleo
- Ukosefu wa dawa hosipitalini
- Ukosefu wa lishe bora
- utegemezi wa misaada
- ukaragosi
- uongozi mbaya
- propaganda
- matumizi mabaya vyombo vya dola
- kutowajibika kwa viongizi
- mishahara duni
- ubadhirifu
- unafiki wa kidini
- ushauri mbaya
- ujinga wa wananchi
- uzalendo wa kijinga
- Mapinduzi
- wafanya kazi kujiuzulu
- migomo ya wafanyi kazi
- mapendeleo kazini
- Ukosefu wa maji safi

Zozote 10 x 2 = 20 (maelezo ni lazima)

SEHEMU YA C: RIWAYA

4. SWALI: Mwanamke amesawiriwa vipi katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea? (al 20)

(a) Mtazamo chanya

- ✓ Mwanamke ni jasiri – Imani alimkabili Mwalimu Majisifu na kumsaili kwa kusoma barua za watu wengine. Pia alimwuliza waziwazi kwa kusema

‘Kumbe wewe si mwandishi?”

Mamake Imani alivyokitetea kishamba chake.

- ✓ Ni mvumilivu – Bi. Zuhura alikaa maisha ya dhiki na kudunishwa na mumewe Nasaba

Bora hadi alipopewa talaka. Dora alionyesha stahamala kubwa kuwatunza wanawe walemavu hata mwalimu Majisifu akawa anamhurumia.

- ✓ Ni mkombozi – Imani anashirikiana na Amani katika kuzungumzia masuala ya ukombozi.

Vilevile, pamoja na Amani aliwakomboa wakazi wa Sokomoko kutokana na imani yao iliyowanyima kunywa maji ya mto Kiberenge.

- ✓ Ni mzalendo – wanawake wengi walihudhuria sikukuu ya wazalendo wakiwemo vikongwe

na wajawazito.

- ✓ Ni mfanyikazi /mwenye bidii – Imani alifanya kazi kwa kujitolea nyumbani kwa mwalimu Majisifu ingawa alilipwa ujira mdogo. Wale wauguzi walioajiriwa zahanati ya Nasaba Bora.
- ✓ Ni mlezi bora – Dora ingawa aliungulika moyoni kwa kujaliwa watoto walemavu, aliwatunza vyema hata hapo alipokosa msaidizi. Mamake Imani aliwashughulikia wanawe baada ya kifo cha mumewe.
- ✓ Msamehevu – Zuhura anahudhuria mazishi ya mumewe japo alikuwa ametalikiwa .
- ✓ Mwenye maadili – Imani kuishi chumba kimoja na Amani pasi na kushiriki mapenzi.
- ✓ Mwenye utu – Zuhura anamwonea imani mwanamke anajifungulia njiani.

(hoja zozote 5 x 2 = 10)

(b) Mtazamo hasi

- ✓ Chombo cha kutosheleza uchu wa mwanaume - Mtemi Nasaba Bora alimtumia Lowela.
- ✓ Kiumbe msumbufu – Michelle mwanamke wa Kifaransa alithamini mali zaidi ya alivyompenda Majinuni.
- ✓ Kiumbe dhaifu – Bi. Zuhura alimwogopa mumewe; asingeweza kujitetea.
- ✓ Katili /Asiye na utu – Lowela alitelekeza kitoto chake Uhuru na kukubaliana na Mtemi Nasaba Bora kuiweka siri.
- ✓ Mvunja nyumba za wengine – wanawake wanaoshiriki mapenzi na Mtemi huku wakijua ana mke.
- ✓ Mpenda anasa – Lowela anaacha shule akiwa kidato cha tatu ili akaponde raha na Mtemi.
- ✓ Asiye na haki – mamake Imani anapigwa na hatimaye kuuliwa kwa sababu ya kijishamba cha mumewe.
  Zozote 5 x 2 = 10

5. a) Mnenaji- Amani

Mnenewa – Imani
Mahali – kibandani mwa Amani
Imani alikuwa amemwambia mengi kujihusu lakini Amani hukuwa amsema lolote kujihusu.
Amani analalamikia jinsi wanyonge hunyimwa haki zao
(zozote 4 x 1 = 4)

b)Tamathali

- Uhaishaji/ uhuishi –dunia inawapuuuza na kuwadunisha
- Msemo – asili wala fasili
- Tabaini – si chochote si lolote (kutambua tamathali al 1, kutoa mfano al 1 = 2 x3)

c)Ni sharti mtahiniwa amtambue mnenaji – Amani- la sivyo asituzwe chochote.)

Usiri wa Amani

- Hakumwambia yeyote sababu yake ya kwenda Sokomoko.
- Amani alijua kuwa Mtemi Nasaba Bora ndiye aliyemuua chichiri Hamadi lakini hakumwambia yeyote.
- Amani alijua kuwa Yusuf Hamadi alisingiziwa mauaji ya Chiriri Hamadi na kisha akafungishwa jela na Nasaba Bora lakini hii ilibaki kuwa siri yake pekee.
- Alikataa kumwambia Imani kuwa alichokitupa katika Ziwa Mawewa ulikuwa mswada wake ulioibiwa na na Mwalimu majisifu. Anamfichulia siri hii baadaye kupitia barua.
- Alishuku kuwa mwizi wa mswada wake alikuwa Mwalimu Majisifu lakini hakuwahi kumwambia yeyote.
- Hakumwambia yeyote kuwa amesoma hadi chuo kikuu lakini Madhubuti anakuja kujijulia kivyake.
- Aliiweka siri sababu yake ya kutaka kuajiriwa kazi kwa Mtemi Nasaba Bora.
- Hakuwa amemwambia yeyote kuwa aliwahi kufungwa jela maiaka mitano .
- Sababu ya Amani ya kurudi kazi kwa Mtemi baada ya makuruhu aliyomtendea ilibaki siri kwake yeye Amani na hakumwambia yeyote.

Zozote 7 x 1 = 7

d)Mnenewa ni Imani.(mtahiniwa asipomtambua kwa jina asituzwe chochote)

Uanamapinduzi wake:

- Alikuwa wa kwanza kuyanywa maji yam to Kibenge, jambo lililokuwa mwiko hapo mbeleni. Tangu siku hiyo wakazi wa Sokomoko wakaanza kuyanywa maji hayo.
- Aliwa wa kwanza kuwatunza watoto walemavu wa Mwalimu Majisifu kwa mapenzi na kuwathamini kama binadamu.
- Aliishi nyumba moja na Amani bila kushiriki mapenzi kama ilivyo desturi ya vijana wengi. (hoja 3 x 1 = 3)

SEHEMU YA D: USHAIRI

6. (a) Dhamira ya shairi.

- Shairi hili linadhamiria kueleza madhara ya kutofuata mawaidha / ushauri wa baba na mama.

- Kuonyesha hasara / shida zinazowapata watu walio na kiburi, majivuno, majigambo, na tamaa.

(Hoja 2 x 1 =alama 2)

(b) Kusisitiza ujumbe.

- Matumizi ya kibwagizo.

- Matumizi ya methali au jazanda. Hoja 1 x 2 = alama 2

(c) Tamathali za usemi

- Swali la balagha – ya nini kushangaa?

- Methali – majuto ni mjukuu huja kinyume.

- Jazanda – Umelichimba la kukuzika handaki

- Istiari – Ulijidhania simba. Zozote 2 x 2 =alama 4

(d) Lugha nathari.

Yale uliyoyaona kuwa bora ndiyo sasa yamekuletea shida. Mamia ya matatizo hayaishi kwako. Iwapo ungetambua hapo awali basi hungekuwa ukitatizika. Wewe mwenyewe ndiye chanzo cha haya. 4 x 1 = alama 4

(e) Idhini ya kishairi

Inkisari – Alikwamba badala ya alikwambia

- Ulodhania badala ya uliyoyadhania.

Kuboronga sarufi – Alikwamba wako mama badala ya alikwambia mama yako

- Umelichimba la kukuzika handaki badala ya umelichimba handaki la kukuzika.

Lahaja – Huaziriki

Zozote 2 x 2 =alama 4

(f) Toni ya shairi hili.

Toni ya masuto/kushutumu / ya kulaumu/ kukejeli – uliyataka mwenywe /ulijiona/ umepatikana Yoyote 1 x 2 = alama 2

(g) Matumizi ya maneno

(i) Mstahiki – mheshimiwa

(ii) Hupuliki – husikii / husikizi (alama 2 x 1 =2)

7.a) shairi huru al 1

Sababu:-halina urari wa vina

- Halina urari wa mizani kwenye mishororo (hoja 2 x 1 =2)

b)-kuweko kwa wizi

kuweko kwa sheria

kuweko kwa wanyonge na matajiri

kuweko kwa njaa (hoja 4 x 1= 4)

c)ubeti wa saba kwa lugha ya nathari

Uzee hutokana na kuweko kwa hali ya ujana. Vivyo hivyo kutokuweko kwa wanaotawaliwa kumesababisha kumalizika kwa utawala. (al 4)

d)mbinu ya uhuru wa kishairi iliyotumika

inkisari al 1.mifano:wanafu-wanafunzi,al 1 'singekuwako- kusingekuwako al 1

e)maana ya maneno

sawa-kamilifu/waadilifu

komeo –kifaa cha kufungia mlango

kutaanasi – kushiriki mambo yanayofurahisha/yanayosrarehesha. (3 x 1 = 3)

SEHEMU YA E: HADITHI FUPI

8.a) Muktadha

-Uzungumzi nafsi wa Abu

- yuko nyumbani kwa akina Amali

- ni siku ya arusi yake na Amali

- sasa hivi ameingia chumbani alimofungiwa bi arusi - Amali

-baadaye alikataa kumuoa Amali (hoja 4 x 1 =4)

b) sharti mtahiniwa ataje anwani ya hadithi – Ndoa ya Samani.

Maana :ndoa ambayo msingi wake si mapenzi ya dhati bali tamaa ya mali/rasilmali/utajiri

- ✓ Mamake Amali alikataa kumuoza Abu bintiye mara ya kwanza kwa kuwa Abu alikuwa maskini wakati huo.
- ✓ Abu alipopeleka posa mara ya pili alikubaliwa kwa kuwa mara hii alikuwa ametengeneza pesa huko Arabuni.
- ✓ Abu alilazimika kulihonga jitu lililojiita kakake bi arusi ili limruhusukuingia chumbani mwa alimofungiwa Amali.
- ✓ Sebuleni mwa akina Amali mmejaa samani alizokuwa amenunua Abu mwenyewe.
- ✓ Amali alimpatia Abu orodha ndefu ya vitu vya thamani ya juu ikiwemo samani kutoka Arabuni vinunuliwe kabla ya arusi kufanyika.
- ✓ Mamake Amali alishurutisha bintiye afanyiwe arusi ya "ndovu kumla mwanawe" (kubwa ya kutajika.
- ✓ Wazazi wa Abu hawakuhusishwa kamwe katika maandalizi wala arusi , labda kutokana na ufukara wao.
- ✓ Abu alitimiza mahitaji yote ya wakweze ingawa shingo upande kwa kuwa aliyaona kuwa ubadhirifu mkubwa. (uk 88)
- ✓ Abu mwenyewe anasema kuwa hukumuoa Amali bali Amali alikuwa ameolewa na mali yake (Abu) "sitaki kusikia Amali na ndoa yake ya samani." Uk 89
- ✓ Mamake Amali alitaka sherehe zote zifanyike kwake badala ya kwa bwana arusi.

Hoja zozote 8 x 2 = 16